**SH. BILIONI TANO << Fedha ambazo mkandarasi wa machinjio ya Vingunguti anatakiwa kulipwa**

# Manispaa Ilala yaagizwa kumlipa mkandarasi

**NA MWANDISHI WETU**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imemtaka mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala, kuhakikisha ndani ya siku saba anamlipa mkandarasi anayejenga machinjio ya Vingunguti sh. bilioni tano anazodai ili akamilishe ujenzi huo.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Pauline Gekul, alipotembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa machinjio hayo, jijini Dar es Salaam.

Pauline alisema hali za machinjio mengi kwa sasa siyo nzuri, wanyama wanachinjwa katika mazingira machafu si salama kwa walaji.

"Machinjio haya ya Vingunguti yatakuwa mkombozi kwa wananchi wa Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla.

"Kwa hiyo mkurugenzi hakikisha ndani ya siku saba, kuanzia leo (juzi) unamlipa mkandarasi ili kazi hii ikamilike kama ambavyo Rais, Dk. John Magufuli alivyoagiza," alisema Gekul.

Alisema kukamilika kwa ujenzi huo ni lazima uende sambamba na ununuzi wa magari kwa ajili ya kubebea nyama na kuzisambaza katika mabucha yaliyopo jijini Dar es Salaam kwa kuwa haitapendeza kuwepo kwa machinjio mazuri halafu nyama zinabebwa kwa kutumia pikipiki.

Alisema ili kuhakikisha machinjio hayo yanapata wanyama wazuri na salama kwa ajili ya walaji, wataboresha mnada wa machinjio ya Pugu, ili wanyama watakaokuwa wanapelekwa hapo wawe na viwango vya kuchakatwa katika machinjio hayo.

Pia, aliwapongeza mkurugenzi na mkandarasi kwa jitihada kubwa wanazozifanya katika kukamilisha ujenzi huo na kuwataka kuongeza kasi ya ujenzi ili ukamilike kama inavyotarajiwa.

Msimamizi wa ujenzi huo kutoka Shirika la Nyumba la Taifa, Mhandisi, Efraim Phanuel, alisema endapo watalipwa fedha wanazodai, watakamilisha ujenzi huo mapema Februari, mwaka huu.

**MNADANI**



**NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (katikati), akikagua stakabadhi ya mteja aliyenunua mbuzi katika mnada wa Pugu, jijini Dar es Salaam. Kulia ni Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama, Imani Sichwale. (Picha na Wizara ya Mifugo).**

# Ujenzi wa nyumba kupigwa 'stop'.

**NA MICHAEL KATONA, NJOMBE**

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Mhandisi Marwa Rubirya, ameiagiza Halmashauri ya Mji wa Njombe, kusimamisha utoaji wa vibali vya ujenzi wa nyumba zilizopo jirani na uwanja wa ndege mkoani humo.

Agizo hilo alilitoa alipokuwa akiongoza kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Njombe, ambapo aliitaka halmashauri hiyo kusitisha utoaji wa vibali vya ujenzi mara moja.

"Ukisoma Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), uwanja wa ndege wa Njombe ni miongoni mwa viwanja ambavyo viko katika mpango wa kujengwa upya.

"Sasa tukiruhusu wananchi waendelee kujenga, sisi wenyewe tutakuwa tunakwamisha utekelezaji wa mradi huu," alisema Rubirya.

Alitoa maelekezo kwa halmashauri ya mji huo, kusitisha utoaji wa vibali na wahakikishe kuwa hakuna ujenzi unaoendelea katika eneo la uwanja wa huo kwa hivi sasa.

"Kwa sababu hadi sasa eneo pekee ambalo limekubalika uwanja wa ndege utajengwa ni hapo ulipo uwanja huo, hatujawa na uamuzi mbadala, kama yatatokea basi eneo hilo tutalibadilishia matumizi na litatumika kwa shughuli nyingine, lakini kwa sababu hatujawa na mabadiliko ya matumizi ni bora tukazingatia maelekezo haya," alisema.

Akizungumzia juu ya wananchi kuendelea kujenga nyumba jirani na uwanja huo, Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Ruth Msafiri, alisema wapo wananchi ambao wanaendelea kukarabati nyumba zao, wengine wanajenga kwa kuwa suala hilo la ujenzi wa uwanja wa ndege kwa kiwango cha lami, limekuwa likizungumzwa kwa muda mrefu sasa.

"Tunaliona kwa namna moja au nyingine jambo hili linaleta mgogoro, tungetamani kuona sasa watu wote waelewe kama kuna tamko lisitishe ili watu waelewe na waache kuendeleza

Scanned with CamScanner



*Mhandisi Efraim Phanuel akimuonesha Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul michoro inayoonesha muonekano wa machinjio ya Vingunguti utakavyokuwa baada ya kukamilika kwake alipotembelea machinjio hayo.*

JAMVI LA HABARI JAN 10, 2021

Scanned with CamScanner

MWANANCHI JAN 10, 2021

# DED Ilala apewa siku saba kumlipa mkandarasi

Bakari Kiango, Mwananchi
bkiango@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul amemtaka Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, Jumanne Shauri kuhakikisha ndani ya siku saba anamlipa mkandarasi anayejenga machinjio ya Vingunguti Sh5 bilioni anazodai kusudi akamilishe ujenzi huo.

Gekul alitoa agizo hilo juzi jioni alipokagua maendeleo ya ujenzi wa machinjio hayo jijini hapa.

Alisema hali ya machinjio nyingi kwa sasa sio nzuri, wanyama wanachinjwa kwenye mazingira machafu yasiyo salama kwa walaji.

Gekul alisema machinjio hayo ya Vingunguti yatakuwa mkombozi kwa wananchi wa Dar es Salaam na Tanzania kwa jumla.

"Kwa hiyo Mkurugenzi hakikisha ndani ya siku saba kuanzia leo (juzi) unamlipa Mkandarasi ili kazi hii ikamilike kama ambavyo Rais, John Magufuli aliagiza," alisema Gekul.

Alisisitiza kukamilika kwa ujenzi huo lazima kuende sambamba na ununuzi wa magari ya kubebea nyama na kuzisambaza kwenye mabucha yaliyopo jijini Dar es Salaam.

Alisema haitapendeza kuwapo kwa machinjio hayo mazuri halafu nyama ziwe zinabebwa kwenye pikipiki.

Naibu waziri huyo alisema ili kuhakikisha machinjio hayo yanapata wanyama wazuri na salama kwa walaji, wataboresha mnada wa machinjio ya Pugu, wanyama watakaokuwa wanapelekwa hapo wawe na viwango vya kuchakatwa katika machinjio hayo.

Pia, aliwapongeza mkurugenzi na mkandarasi kwa jitihada kubwa wanazozifanya katika kukamilisha ujenzi huo na kuwataka kuongeza kasi ya ujenzi ili ukamilike kama inavyotarajiwa.

Msimamizi wa ujenzi huo kutoka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Mhandisi, Efraim Phanuel alisema endapo watalipwa fedha wanazodai kama alivyoagiza Naibu Waziri watakamilisha ujenzi huo mapema mwezi wa pili mwaka huu.

Scanned with CamScanner

Jumapili Januari 10 - 16, 2021 | MZALENDO



Scanned with CamScanner

# Gekul gives Ilala director seven –day ultimatum

By SUNDAY NEWS Reporter

THE Deputy Minister of Livestock and Fisheries, Ms Pauline Gekul has issued a seven-day ultimatum to Ilala District Executive Director to clear a sum of 5bn/-owed by the contractor of Vingunguti abattoir for completion of the project.

Ms Gekul issued the ultimatum when she went to inspect the development of the project recently in Dar es Salaam.

She said animals are currently being slaughtered in unsafe environment because the condition of most slaughter houses is not encouraging, citing that the Vingunguti abattoir is going to be a savior to the whole country, particularly Dar es Salaam.

"The DED should ensure the money is paid within seven days from (today) Friday for the job to be completed as per President John Magufuli's directive," said Ms Gekul.

She emphasized that completion of the project should go hand in hand with the procurement of special vehicles for supplying meat.

> **Aanimals are currently being slaughtered in unsafe environment because the condition of most slaughter houses is not encouraging, citing that the Vingunguti abattoir is going to be a savior to the whole country, particularly Dar es Salaam.**

SUNDAY NEWS JAN.10, 2021



Ms Gekul



Mr Ulega

According to her, it will not make sense having a good abattoir while meat is still supplied in the butchers using 'boda bodas'.

She said Pugu auction will undergo major improvement to ensure the abattoir has access to a good and quality animal supply to cater for the demands of consumers.

The Deputy Minister applauded the DED and contractor for the huge efforts being put in finalizing the project, urging them to speed up the construction.

The Project Supervisor from the National Housing Corporation, Eng Efraim Phanuel pledged to ensure the project is completed by February if the minister's directive is implemented.

Last year when the former Deputy Minister for Livestock and Fisheries, Mr Abdallah Ulega made a tour of the abattoir, he said the popular slaughter house will serve Dar es residents, neighbouring regions as well as importing meat to neighbouring countries.

"Completion of this facility will increase meat supply and sell outside the country, including in Arab nations," Mr Ulega said.

Among other factors, the slaughterhouse is strategically positioned since it is located near the Julius Nyerere International Airport (JNIA), which makes it easy to transport the meat.

Mr Ulega encouraged local investors with capital to invest in cold storage facilities at the new abattoir, saying it will be another opportunity for investors.

The new facility will have a capacity to slaughter 1500 cows and 1000 goats every day.

The country has been spending over 10bn/- on importing meat, but the deputy minister expressed hopes that the construction of the new abattoir will completely end importation of meat.

This is despite the fact that Tanzania has a high population of cows and goats, totalling 35 million and 20 million, respectively.

Scanned with CamScanner

# Halmashauri zashauriwa kutumia BMU kukusanya mapato ya uvuvi



*Mratibu wa Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali za Bahari Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish), Dk. Nichrous Mlalila akimueleza jambo Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (kushoto) alipotembelea kukagua maendeleo ya ujenzi wa ofisi ya Kikundi cha Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU) inayojengwa katika Kata ya Dunda, Wilayani Bagamoyo Januari 7, 2021.*



*Mwenyekiti wa Kikundi cha Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU), Kata ya Dunda, Wilayani Bagamoyo, Isihaka Hudi (kulia) akimueleza jambo Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (kushoto) alipotembelea kukagua maendeleo ya ujenzi wa Ofisi ya BMU hiyo Januari 7, 2021.*



*Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (kushoto) akitoa maelekezo kwa Mratibu wa Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali za Bahari Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish), Dk. Nichrous Mlalila ( kulia) alipotembelea kukagua maendeleo ya ujenzi wa ofisi ya Kikundi Cha Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU) katika kata ya Dunda, Wilayani Bagamoyo Januari 7, 2021.*

NA MBARAKA KAMBONA

KAZI kubwa ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kujenga mazingira bora yatakayowafanya wananchi wake waweze kujizalishia kipatoa lakini pia kuongeza pato la taifa kwa kulipa kodi.

Kutokana na mazingira hayo, Serikali imeamua kuzihamasisha Halmashauri kwa kuzipa kupitia wananchi husika kukusanya mapato ili kuziwezesha kupata kipato cha uhakika cha kuendesha shughuli zao za kulinda rasilimali.

Hivi karibuni Mratibu wa Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali za Bahari Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish), Dk. Nichrous Mlalila aliziomba Halmashauri kuvitambua Vikundi vya Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU).

Lakini pia kuzipa uwezo wa kukusanya mapato yatokanayo na shughuli za uvuvi ili ziweze kusaidia vikundi hivyo kujiendesha na kuendeleza sekta ya uvuvi nchini.

Dkt. Mlalila alitoa rai hiyo katika ziara ya Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul alipotembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa ofisi ya BMU inayojengwa na Mradi wa SWIOFish katika Kata ya Dunda, Wilayani Bagamoyo Januari 7, 2021.

Kwa mujibu wa Dkt. Mlalila sehemu kubwa ya mapato yanayokusanywa kwa sasa na Halmashauri hayarudishwi kwa Jamii ya wavuvi kwa ajili ya kuendeleza shughuli za sekta na uchumi wa jamii husika.

Dkt. Mlalila anasema anatambua kuwa kuna changamoto ya kisheria ambayo baadhi ya Halmashauri zimetumia kuzizuia BMU kukusanya mapato yanayotokana na rasilimali za uvuvi.

"Tunahamasisha Halmashauri kuwapa uwezo BMU kukusanya mapato ili kuziwezesha kupata kipato cha uhakika cha kuendesha shughuli zao za kulinda rasilimali za Uvuvi lakini pia mapato hayo yatawezesha kuendeleza sekta ya uvuvi tofauti na ilivyo sasa,"anasema Dk. Mlalila.

Katika baadhi ya Halmashauri ambazo wamewapa kazi BMU ya kukusanya mapato kama vile Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, Mkoani Tanga, Mapato yanayotokana na uvuvi yameongezeka kutoka shilingi milioni 9 kwa robo mwaka hadi milioni 51 na kutoka shilingi milioni 36 hadi milioni 256 kwa mwaka.

"Nazishauri Halmashauri nyingine zichukue mfano wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani kwa sababu sisi tumezipa mafunzo ya kina hizi BMU katika kusimamia fedha na ukusanyaji wa mapato, hivyo tunaamini hilo ni suala la mchakato na tumewasilisha andiko TAMISEMI ili kuangalia namna ya kuzifanya BMU kuendelea na shughuli zake hata pale ambapo mradi wa SWIOFish utakapokwisha muda wake,"anaongeza Dk. Mlalila.

Akizungumzia suala hilo, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul alisema "BMU ya Kata ya Dunda na zingine zikajifunze Pangani kuona wao wanafanyaje na sisi kama Wizara tutaangalia kama kuna chanzo ambacho wataalam wa Halmashauri wanakusanya na hakifanyi vizuri na kuna BMU mahali inakusanya vizuri basi tuaibua hiyo hoja tuone tutafanyaje.

"Ukweli ni kwamba kwenye vyanzo hivi vya leseni na ushuru wa rasilimali za uvuvi katika halmashauri zetu nyingi hazifanyi vizuri na hivyo kuna haja ya kuviangalia vizuri hasa wataalam wetu wanaotumika kukusanya hayo mapato kwa sababu kuna baadhi yao wamefanya hapo ndio maeneo yao ya kupatia pesa zao,"anasema Gekul.

Gekul, anasema Wakurugenzi wanaweza kuwa na nia njema kabisa lakini wale wanaotumwa kukusanya hayo mapato wanarudisha maduhuli hayo kama walivyotumwa?

Anasema kama kuna watu wanauwezo wa kukusanya zaidi ya wataalam wa Halmashauri sidhani kama kuna haja ya kuwa na kigugumizi cha kuwatoa hao watu ili kazi hiyo apewe anayeweza kukusanya vizuri. "Kwa sababu mwisho wa siku sisi wananchi tunachotaka ni maendeleo hivyo nisingependa niseme moja kwa moja hapa kuwa BMU wapewe kazi hiyo isipokuwa Halmashauri ziangalie kama sheria inawaruhusu kuwatumia BMU kukusanya mapato,"anaongeza Gekul.

Gekul, anasema kuwa wao kama Wizara watawasiliana na TAMISEMI kuona maelekezo yakoje kwa sababu anasema kuna vyanzo Halmashauri zenyewe zinakusanya na vingine vinaruhusiwa kukusanywa na wakala na pale ambapo BMU itaonekana inafaa ipewe uwezo wa kukusanya.

Mradi wa SWIOFish unafadhiliwa na Benki ya Dunia kuhamasisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za bahari na ndio umeimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi wa rasilimali za bahari (BMU) kwa ajili ya kulinda na kuhamasisha uvunaji endelevu wa rasilimali za bahari katika Wilaya za Mkinga, Pangani, Bagamoyo, Lindi Vijijini na Tanga Jiji.

Scanned with CamScanner

# Nine people arraigned for stealing cashew nuts

From ANNE ROBI in Mtwara

NINE people have been arraigned for allegedly stealing 1,515 sacks of raw cashew nuts worth 163.9m/- from Yalin Cashew Nut Company Store situated in Msijute Industrial Area in Mtwara Region.

Speaking on the incident, Mtwara Regional Police Commander Mark Njera said the suspects had been arraigned for allegedly breaking into the cashew nut warehouse and stealing the cashew nuts.

The incident occurred between September and October last year, adding that the suspects were later taken to court on December 24 and were charged with stealing 105,725kg.

The RPC named those arraigned as Yusuf Lupalale (40), Issa Chitanda (24), Ally Seleman (27), Faraji Zungu (36), Hamza Bonge (32), Mudy Jaba (27), Hassan Ndolomi (36), Abdilah Ndunga (28) and John Nyoni (34). He said the police were still hunting for others in connection with the theft and he warned other people against ... illegal business



*TANZANIA Fishing Corporation (Tafico) fishing consultant from Japan Koji Hase shows Deputy Minister for Livestock and Fisheries Pauline Gekul (right) some information on fishing when she visited Tafico offices in Dar es Salaam yesterday.(Photo by Ministry)*

# VP urges women lawyers to fight for women's rights

From SULEIMAN

from the Judiciary of Tanzania. ... said the gov-

give recommendations to be incorporated in the five-year stra-

noted that as they celebrated the 20th anniversary of TAWJA, they had recorded roaring suc-

Scanned with CamScanner

# Halmashauri zashauriwa kutambua BMU

Na Mwandishi Maalumu

MRATIBU wa Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali za Bahari Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish), Dk Nichrous Mlalila ameziomba halmashauri kuvitambua vikundi vya ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU).

Aidha amezitaka halmashauri hizo kuzipa uwezo wa kukusanya mapato yatokanayo na shughuli za uvuvi zisaidie vikundi hivyo kujiendesha na kuendeleza sekta ya uvuvi nchini.

Mlalila alitoa rai hiyo katika ziara ya Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul alipotembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa ofisi ya BMU inayojengwa na Mradi wa SWIOFish katika Kata ya Dunda, wilayani Bagamoyo Januari 7, 2021.

Alisema sehemu kubwa ya mapato yanayokusanywa kwa sasa na Halmashauri hayarudishwi kwa Jamii ya wavuvi kwa ajili ya kuendeleza shughuli za sekta na uchumi wa jamii husika.

Mlalila alisema anatambua kuwa kuna changamoto ya kisheria ambayo baadhi ya halmashauri zimetumia kuzizuia BMU kukusanya mapato yanayotokana na rasilimali za uvuvi.

"Tunahamasisha halmashauri kuwapa uwezo BMU kukusanya mapato ili kuziwezesha kupata kipato cha uhakika cha kuendesha shughuli zao za kulinda rasilimali za uvuvi lakini pia mapato hayo yatawezesha kuendeleza sekta ya uvuvi tofauti na ilivyo sasa," alisema Mlalila

Katika baadhi ya halmashauri ambazo wamewapa kazi BMU ya kukusanya mapato kama vile Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, Mkoani Tanga, Mapato yanayotokana na uvuvi yameongezeka kutoka Sh milioni tisa kwa robo mwaka hadi milioni 51 na kutoka Sh milioni 36 hadi milioni 256 kwa mwaka.

"Nashauri halmashauri nyingine zichukue mfano wa halmashauri ya Wilaya ya Pangani kwa sababu sisi tumezipa mafunzo ya kina hizi BMU katika kusimamia fedha na ukusanyaji wa mapato, hivyo tunaamini hilo ni suala la mchakato na tumewasilisha andiko Tamisemi ili kuangalia namna ya kuzifanya BMU kuendelea na shughuli zake hata pale ambapo mradi wa SWIOFish utakapokwisha muda wake," alisema Mlalila

The Guardian

# BMUs important for development of fisheries sub-sector - Dr Mlalila

By Guardian Correspondent

THE government has called upon district councils should learn beach management units (BMUs) in their specific areas and use them to enhance revenue collections from fishing activities.

The coordinator of the South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth (SWIOFish) project under the Ministry of Livestock and Fisheries, Dr Nichrous Mlalila, has said the BMUs are important for development of the fishing sub-sector.

He made the statement on Thursday when briefing the Livestock and Fisheries Deputy Minister, Pauline Gekul who was inspecting construction progress of BMU office at Dunda ward in Bagamoyo District, Coast Region with support from the SWIOFish project under the World Bank.

Dr Mlalila was concerned that collected revenues are currently spent by the district councils instead of being returned to the BMUs which are responsible of managing the beach areas as well as ensuring sustainable fishing activities.

He however noted that there are some legal challenges which prohibit BMUs from collecting revenues from marine resources.

"We encourage district councils to allow BMUs to collect revenues and use them to develop their fishing activities. These revenues will be directly spent to improve the fishing sector," Dr Mlalila noted.

He added that in district where the BMUs have been allowed to collect revenues, collections have increased tremendously.

He gave an example of Pangani District in Tanga Region where collections increased from 36m/- to 256m/- per year.

Under World Bank funded project, fifty BMU groups were established in Pangani, Bagamoyo, Mkinga, Tanga Urban, and Lindi Rural districts and before venturing into the new task of collecting revenues, members of fishery units were trained on how better to do the job.

The task was part of empowering members with financial muscles.

Through the six-year project, construction of BMU offices are in different stages of construction including Mkinga District at Zingibari, Pangani (Kipumbwi), Lindi Rural (Sudi), Bagamoyo (Dunda), and Chalinze (Saadani)

The deputy minister urged other BUMs to learn from the Pangani BMU to enhance their revenue collections.

Gekul highlighted the need for district authorities to closely monitor officers' in-charge of collecting levies from fishing activities because some of the funds end up in individual pockets.

"BMUs should be tasked to collect revenues, but this should be done on legal agreements. We will consult the President's Office - Regional Administration and Local Government for guidelines," said Gekul.

SWIOfish is the World Bank funded 'South-west Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth Project' for the Africa region with the aim to improve the management effectiveness of selected priority fisheries at the regional, national and community level.

In Tanzania, the programme is jointly implemented by the Ministry of Livestock and Fisheries, Ministry of Agriculture, Natural Resources, Livestock and Fisheries (Zanzibar) and the Deep Sea Fishing Authority (DSFA) focuses on six priority fish species.

Scanned with CamScanner